

21 Februari 2024

## **Heshima ya ‘Kipekee’: Shule ya Robert Shaw Theme yatambuliwa kama Mojawapo ya Shule Bora Zaidi Kitaifa**

Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb ina furaha kutangaza kwamba Robert Shaw Traditional Theme School imechaguliwa kama Shule ya Kipekee ya 2023 kulingana na Sheria ya Kitaifa ya Shule za Msingi na Sekondari (*ESEA*). Heshima hii ni uthibitisho wa bidii na ari ya wanafunzi, walimu na wafanyakazi katika kutoa elimu ya kiwango cha kimataifa kila siku.

Chama cha Kitaifa cha Wasimamizi wa Mpango ESEA wa Jimbo (National Association of ESEA State Program Administrators, *NAESPA*) hutoa heshima ya kitaifa kwa shule mbili kati ya zilizofanya vizuri zaidi za mpango wa Title I katika kila jimbo. Katika Georgia, asilimia tano ya shule za mpango wa Title I zilizofanya vizuri zaidi, kulingana na alama zilizounganishwa za ELA na Kiwango cha Mafanikio ya Hisabati, zinastahiki kutuma maombi ya kupokea tuzo hii.

“Haya ni mafanikio bora kwa Robert Shaw Traditional Theme School! Inaonyesha kwa uthabiti ubora wa kimasomo, ufaulu wa wanafunzi, na kujitolea kwa maadili yetu ya msingi, na hivyo kuendeleza juhudhi zetu za *Kufanya Mambo Tofauti ili Kuleta Ubora*,” Msimamizi wa DCSD Dkt. Devon Q. Horton alisema.

“Robert Shaw Traditional Theme School imepiga hatua thabiti kutoa elimu bora kwa kila mwanafunzi inayomhudumia,” Msimamizi wa Shule za Jimbo Richard Woods alisema. “Ninawapongeza kwa dhati kitivo, wafanyakazi, wanafunzi na wazazi wa Robert Shaw Traditional Theme School kwa heshima hii wanaostahiki ya kitaifa. Ninawashukuru kwa kuiwakilisha Georgia vyema kwenye jukwaa la kitaifa.”

Robert Shaw alitunukiwa ruzuku ya \$20,000 na Mpango wa Part A wa Title I ya Idara ya Elimu ya Georgia Ruzuku hii itatumika kulipia gharama za usajili za timu ya shule kuhudhuria Kongamano la Kitaifa la ESEA mwaka wa 2024 na kusaidia miradi ya mpango wa Title I.

NAESPA imetambua kila Shule ya Kipekee ya Kitaifa ya ESEA kwa kuwapa kifurushi maalum cha tuzo, sehemu maalum kwenye tovuti ya Mtandao wa ESEA, na wasilisho maalum katika Kongamano la Kitaifa la ESEA, ambalo lilifanyika mapema mwezi huu katika Portland, Oregon.

Kongamano hili lilijumuisha vipindi maalum vilivyoonyesha Hadithi za Mafanikio kutoka kwa Shule za Kipekee, vikiangazia kazi yao nzuri ili kuboresha ubora wa elimu ya wanafunzi wao kwa kiasi kikubwa. Wahudhuriaji kutoka Shule hii ya Kipekee walisherehekewa wakati wa hafla kadhaa maalum za kongamano.